Tanzania Airports Authority

Imethibitishwa: ISO 9001:2015, 14001:2015 & 45001:2018

# JARIDA MTANDAO

Toleo Na. 1










"Lango lako kuifikia Dunia"




@tanzaniairports

# YALIYOMO

UK 2. Jengo la Abiria Tabora kuanza kazi rasmi
UK 3. Usalama Usafiri wa Anga kuimarika
UK 4. Naibu Katibu Mkuu Uchukuzi atembelea Kiwanja cha Ndege Sinyanga
UK 5. TAA na TRC watia saini hati ya makubaliano
UK 6. Ulinzi na Usalama Usafiri wa Anga ni wa uhakika
UK 7. Mkurugenzi Mkuu TAA akutana na watumishi.
UK 8. Bodi na Menejimenti TAA wapatiwa mafunzo
UK 9. TAA yalipa fidia waliopisha ujenzi Musoma
UK 10. Mradi wa ukarabati Kiwanja cha Ndege Iringa
UK 11. Matukio katika Picha.
UK 12. Maegesho ya muda mrefu.
UK 13. Watu wetu








## NENO LA MKURUGENZI MKUU

Napenda kutoa shukrani za dhati kwa wadau wote wa sekta ya usafiri wa anga, pamoja na wafanyakazi wa Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania kwa ushirikiano wao mkubwa katika kuendesha, kuendeleza na kuboresha viwanja vya ndege nchini.

Ushirikiano huu umekuwa chachu katika kufanikisha utekelezaji wa majukumu ya Mamlaka kwa ufanisi.

TAA inaendelea kuboresha miundombinu na huduma katika viwanja vya ndege vinavyosimamiwa na Mamlaka kwa kuzingatia ukamilifu wa viwango vya usalama, ubora na huduma za kimataifa, kwa lengo la kuchochea maendeleo ya uchumi, kukuza sekta ya utalii pamoja na kuimarisha biashara na uwekezaji.

TAA inajikita kaitka usimikaji wa mifumo saidizi ili kuboresha huduma za Viwanja vya ndege haswa katika maegesho ya magari, maeneo ya biashara na maegesho ya ndege ili kusimamia huduma hizo kwa ufanisi zaidi.

Aidha, tunaendelea kutoa huduma bora, salama na zenye viwango vya kitaifa na kimataifa kwa kuzingatia mahitaji ya wadau wote na maslahi mapana ya nchi. Kwa kushirikiano kwa karibu na wadau tutaendelea kuimarisha sekta ya usafiri wa anga na kuileta nchi maendeleo endelevu.

Abdul Mombokaleo
Mkurugenzi Mkuu
**Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania**





# JENGO LA ABIRIA KIWANJA CHA NDEGE CHA TABORA KUANZA KAZI





Waziri wa Uchukuzi, Prof. Makame Mbarawa, amekagua na kutembelea jengo la abiria katika kiwanja cha ndege Tabora ambapo ujenzi wake umekamilika kwa sasa.

Akizungumza katika ziara hiyo, Prof. Mbarawa amesema "Nimechagua kuanza ziara yangu Tabora kwa sababu ni Mkoa wa kimkakati. Reli kutoka Makutupora hadi Tabora, Isaka, Mwanza, na Tabora hadi Uvinza, Bunjumbura hadi Congo zote zinaifanya Tabora kuwa kitovu cha usafirishaji wa kimataifa."

Prof. Mbarawa ameeleza kuwa kukamilika kwa jengo hilo la abiria ni hatua muhimu kwa ukuaji wa uchumi na maendeleo ya sekta ya usafiri wa anga nchini.

Kwa upande wake, Mkuu wa Wilaya ya Tabora, kwa niaba ya Mkuu wa Mkoa wa Tabora Pendo Wella, amemshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa mradi huo mkubwa, na kuahidi kuwa Serikali ya Mkoa wa Tabora na wananchi watautunza ipasavyo na kuhakikisha unaleta fursa za kiuchumi kwa wakazi na wawekezaji wa Tabora.

Aidha Mhandisi wa mradi huo Bw. Raphael Stanislaus Mlimabi, ambaye ni Meneja wa TANROADS Mkoa wa Tabora amesema jengo hilo lina uwezo wa kuhudumia abiria 120 kwa wakati mmoja, lina ofisi za idara mbalimbali, maeneo ya biashara, mnara wa kuongozea ndege, mifereji, eneo la maegesho ya magari (magari 54 kwa wakati mmoja), uzio wa usalama wa urefu wa km 6.25, kituo cha hali ya hewa, majenereta mawili (1000kva na 40kva), taa za sola, pamoja na transfoma ya 1250KV.



# SERIKALI KUENDELEA KUIMARISHA USALAMA WA USAFIRI WA ANGA NCHINI

Serikali kupitia Mamlaka ya Viwanja vya ndege Tanzania inaendelea kujenga na kufanya ukarabati wa miundombinu kwenye viwanja vyote vya Ndege nchini ili kuweka mazingira rafiki kwa abiria na wadau wanaotumia usafiri wa anga.



Hayo yamesemwa jijini Dar es Salaam na Naibu Waziri wa Uchukuzi Mhe. David Kihenzile wakati wa kilele cha maadhimisho ya kampeni ya Utamaduni wa Usalama wa Usafiri wa Anga inayoadhimishwa mwishoni mwa kila mwaka duniani.

Maadhimisho haya yametoa fursa ya kipekee ya kutafakari safari ndefu ya kujenga na kuimarisha Utamaduni wa Usalama katika usafiri wa Anga nchini. “ninapofunga maadhimisho haya, hatusherehekei tu kilele cha kampeni hii kwa kutoa elimu bali pia tunathibitisha dhamira ya serikali kuendeleza mazingira salama, thabiti na yenye kuaminika kwa wote wanaotumia huduma za usafiri wa Anga nchini.” Alisema Mhe. Kihenzile.

Aidha Tanzania inashika nafasi ya nne barani Afrika kwa ubora wa ulinzi katika viwanja vya Ndege kupitia ukaguzi uliofanywa na shirika la Kimataifa la Usafiri wa Anga Duniani (ICAO) wa masuala ya ulinzi (ICAO Universal Security Audit Program- Continous Monitoring Approach) kwa kuwa na ufaulu wa asilimia 86.70.



Mwakilishi wa Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania (TAA), Mkurugenzi wa Rasilimali Watu na Utawala, Bi. Irene Minja amesema maadhimisho haya yamelenga kutoa elimu zaidi kwa abiria na wadau mbalimbali katika sekta ya usafiri wa anga ili kuongeza uelewa na kushiriki kikamilifu katika masuala ya usalama ikiwemo kufuata sheria na taratibu na kuhakikisha kunakuwa na mazingira salama kwenye viwanja vya ndege.

Maadhimisho hayo yamebeba kauli mbiu inayosema, “Usalama wa Usafiri wa Anga unaanza na mimi”.



# NAIBU KATIBU MKUU WIZARA YA UCHUKUZI ATEMBELEA KIWANJA CHA NDEGE CHA SHINYANGA

Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Uchukuzi Mhe. Ludovick Nduhiye amepongeza hatua iliyofikiwa katika ujenzi wa Kiwanja cha Ndege cha Shinyanga huku akihimiza kukamilika kwa wakati kwa ujenzi huo ili kiwanja kianze kuhudumia wananchi wa mkoa huo na mikoa jirani.

“Najua kiwanja hiki kimefikia hapa kwa sababu ya kazi yenu nzuri ya usimamizi, lakini hakikisheni kiwanja kinakamilika kwa wakati na thamani ya pesa inaonekana maana hizi ni hela za watanzania zinatumika,” Amesema Mhe. Nduhiye.

Pia Mhe. Nduhiye ameongeza kuwa kukamilika kwa ujenzi wa kiwanja hicho kutachochea kukua kwa uchumi katika nyanja za kilimo, madini pamoja na biashara jambo ambalo ni kipaumbele cha serikali ya awamu ya sita.

Kwa upande wake Meneja wa Wakala wa Barabara Tanzania (Tanroads) Mkoa wa Shinyanga Mhandisi Samweli Mwambungu amesema ujenzi wa mradi huo wenye thamani ya Shilingi bilioni 44 mpaka sasa umefikia asilimia 94.2 ya ujenzi wake.

Mwambungu ameongeza kuwa ujenzi wa njia ya kutua na kurukia ndege (Runway) pamoja na uzio wa kuzunguka kiwanja hicho umekamilika kwa asilimia 100 huku ujenzi wa jengo la abiria ukiwa katika hatua za umaliziaji.

Meneja wa kiwanja hicho Lugano Mwinuka amesema “kama Mamlaka ya Viwanja vya ndege tumejipanga kuwahudumia wananchi mara ujenzi utakapokamilika kwani shughuli zilisitishwa ili kuharakisha kukamilika kwa mradi huo.







# TAA NA TRC WASAINI HATI YA MAKUBALIANO YA USHIRIKIANO USAFIRI WA ANGA NA RELI NCHINI

Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania (TAA) na Shirika la Reli Tanzania (TRC) wamesaini hati ya makubaliano ya kuunganisha usafiri wa anga na reli nchini, hatua iliyolenga kuimarisha huduma kwa abiria na wasafirishaji wa mizigo kwa kuunganisha miundombinu ya viwanja vya ndege na reli.

Makubaliano hayo yamefanyika jijini Dar es Salaam kati ya Mkurugenzi Mkuu wa TAA, Bw. Abdul Mombokaleo, na Mkurugenzi Mkuu wa TRC,
Mha. Machibya Masanja.

Mara baada ya kutia saini hati ya makubaliano Mha. Machibya amesema ushirikiano huo utawezesha wasafiri kuingia na kutoka katika viwanja vya ndege kwa urahisi zaidi kupitia huduma za reli, amebainisha kuwa hatua hiyo ni utekelezaji wa maelekezo ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe, Dkt, Samia Suluhu Hassan aliyoyatoa wakati wa uzinduzi wa Bandari ya Kwala, ambapo aliagiza TRC kufungua vituo vyenye miundombinu itakayowezesha kuunganisha reli na viwanja vya ndege.

"Kwa sasa upembuzi yakinifu katika Kiwanja cha Ndege cha JNIA umekamilika, na kwa Kiwanja cha Ndege cha Msalato mchakato unaendelea, pia katika Kiwanja cha Ndege cha KIA, tayari kuna miundombinu ya reli ya MGR ambayo itakarabatiwa na kujengwa kituo cha treni".

Mha. Machibya amesema, maboresho haya yatawezesha kukuza shughuli za utalii, kurahisisha usafirishaji wa bidhaa zinazoharibika kwa haraka (perishable goods), na kupunguza gharama kwa wasafiri na wasafirishaji".

Kwa upande wake, Mkurugenzi Mkuu wa TAA Bw. Abdul Mombokaleo amesema ushirikiano huu ni hatua muhimu kwa maendeleo ya taifa kwani utaimarisha sekta ya anga na reli kwa pamoja.

Ushirikiano huo utachangia kukuza uchumi wa nchi, kuongeza pato la Taifa na kuboresha sekta ya usafiri wa anga na reli na kuimarisha ongezeko la abiria na mizigo, Pia utasaidia kuimarisha urahisi wa usafirishaji wa mizigo inayosafirishwa nje ya nchi (export cargo)

Bw. Mombokaleo ameongeza kuwa huduma za kisasa kama remote check-in na drop-off zitatolewa nje ya viwanja vya ndege ambapo zitawezesha usafirishaji wa abiria na mizigo kutoka kwenye vituo vya treni kwenda viwanja vya ndege.






# ULINZI NA USALAMA WA USAFIRI WA ANGA TANZANIA NI WA UHAKIKA

Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania (TAA) imeendelea kujizatiti katika kuboresha miundombinu ya viwanja vya ndege nchini ili kuimarisha mazingira ya utoaji huduma bora, kuongeza ufanisi wa usafiri wa anga, kukuza uchumi na kuchochea pato la taifa.

Wakati wa uzinduzi wa Maadhimisho ya Kampeni ya Utamaduni wa Usalama wa Usafiri wa Anga, Mkurugenzi Mkuu wa TAA, Bw. Abdul Mombokaleo, amesema maboresho ya miundombinu yanakwenda sambamba na kuimarisha mifumo ya kiusalama ili kuendana na mahitaji ya sasa ya sekta ya usafiri wa anga.

"TAA imejipanga kuongeza na kuboresha miundombinu kwenye viwanja vyetu vya ndege ili kuhakikisha tunatoa huduma salama, za kisasa na zenye ufanisi. Kila hatua ya uboreshaji inakwenda sambamba na kuimarisha viwango vya usalama, kwani kadri shughuli za kiwanja zinavyoongezeka, ndivyo inavyotakiwa kuongeza uwezo wa mifumo ya ulinzi na usalama," alisema Bw. Mombokaleo.

Aidha, Mkurugenzi Mkuu ametoa rai kwa wadau wote kushiriki kikamilifu kwenye maonesho na shughuli za wiki hiyo ili kuchangia mawazo, kutoa ushauri na mapendekezo yatakayosaidia kuimarisha usalama na ulinzi katika maeneo yote ya viwanja vya ndege nchini.

Kwa upande wake, Kaimu Mkurugenzi wa Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Julius Nyerere (JNIA), Bi. Bertha Bankwa, amesema Maadhimisho ya kampeni ya Utamaduni wa Usalama wa Usafiri wa Anga yanalenga kuongeza uelewa kwa watumishi, abiria na wadau kuhusu wajibu wa pamoja katika kuimarisha usalama.

"Wiki hii inatukumbusha kuwa usalama si jukumu la kitengo cha usalama pekee au mashine za ukaguzi. Usalama ni jukumu la kila mmoja kama kauli mbiu inavyosema 'Usalama wa Usafiri wa Anga Unaanza na Mimi" na inasisitiza uwajibikaji wa mtu mmoja mmoja katika kulinda usalama," alisema Bi. Bankwa.

Maadhimisho hayo yalilenga kutoa elimu zaidi kwa abiria na wadau mbalimbali katika sekta ya usafiri wa anga ili kuongeza uelewa na kushiriki kikamilifu katika masuala ya usalama ikiwemo kufuata sheria na taratibu na kuhakikisha kunakuwa na mazingira salama kwenye viwanja vya ndege.







# MKURUGENZI MKUU TAA AKUTANA NA WATUMISHI WA MAKAO MAKUU

Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania (TAA), Bw. Abdul Mombokaleo, amefanya mkutano wa ndani wa kwanza kwa mwaka wa Fedha 2025/2026 na wafanyakazi wa Makao Makuu ya TAA na kiwanja cha ndege cha Kimataifa cha Julius Nyerere ikiwa na lengo la kuhimiza uwajibikaji wa kiutumishi katika mifumo ya utendaji kazi, Mafunzo, kuboresha mawasiliano ya ndani na kutoa mwelekeo wa kimkakati wa utendaji wa Mamlaka.

Katika hotuba yake, Mkurugenzi Mkuu amewataka watumishi kuendelea kuzingatia maadili ya kazi, kuheshimu muda na kushiriki kikamilifu katika juhudi za kuboresha huduma za viwanja vya ndege nchini huku akisistiza umuhimu wa mshikamano na ubunifu katika kutekeleza majukumu ya kila siku.

Pamoja na hayo Mkurugenzi Mkuu amewajulisha Watumishi juu ya TAA kujiendesha kibiashara na kuhakikisha inaboresha mifumo ya kiteknolojia ili kuendana na nyakati za kidigitali katika utendaji kazi.

Aidha, Bw. Mombokaleo amepata wasaa wa kuwasikiliza watumishi na kujibu maswali mbalimbali kuhusu mazingira ya kazi, mafao na maendeleo ya kitaaluma, huku akiahidi kushughulikia changamoto zilizowasilishwa kwa wakati na kwa ufanisi.

Mkutano huo umefanyikia katika kwenye ukumbi wa mikutano uliopo katika jengo la tatu la abiria katika Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Julius Nyerere na umehudhuriwa na watumishi wa idara zote, ikiwa ni sehemu ya juhudi za Menejimenti katika kuimarisha mawasiliano ya ndani na kukuza utendaji bora ndani ya taasisi.






# BODI YA MAMLAKA YA VIWANJA VYA NDEGE TANZANIA (TAA) PAMOJA NA MENEJIMENTI WAPATA MAFUNZO MAALUM JUU YA DHANA YA MABADILIKO MAHALI PA KAZI

Bodi ya Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania (TAA) pamoja na Menejimenti wamepata mafunzo ya Dhana ya Utamaduni wa Mabadiliko Mahali pa Kazi (Workplace Culture Transformation)" yaliyofanyika katika Ukumbi wa APC uliopo Bunju, jijini Dar es Salaam.

Mafunzo hayo yamelenga kuwajengea uwezo viongozi hao katika kusimamia mabadiliko chanya ndani ya taasisi, hususani katika kipindi hiki ambacho TAA inaendelea kutekeleza miradi mikubwa ya maendeleo katika viwanja vya ndege nchini, pamoja na maboresho ya mifumo ya kiutendaji, kidigitali, biashara na utoaji wa huduma kwa wateja.

Akifungua mafunzo hayo, Mwenyekiti wa Bodi ya TAA, Bw. Juma Hassan Fimbo, amesema mabadiliko ni sehemu muhimu ya ukuaji wa taasisi yoyote na yanahitaji uelewa wa pamoja, ushirikiano na mawasiliano yenye ufanisi ili kufanikisha malengo ya kimkakati ya Mamlaka.

Kwa upande wake, Mkurugenzi Mkuu wa TAA, Bw. Abdul Athumani Mombokaleo, ameeleza kuwa mafunzo hayo ni sehemu ya mkakati wa kuimarisha utamaduni sahihi wa uongozi (leadership culture) ndani ya TAA, ili kuhakikisha viongozi na watendaji wanakuwa chachu ya mabadiliko endelevu, hasa katika maeneo ya teknolojia, utendaji kazi, biashara na huduma kwa abiria.

Mafunzo hayo ni muendelezo wa kuwajengea uwezo Bodi na Menejimenti ya Mamlaka katika kutekeleza wajibu wake wa kusimamia mabadiliko ndani ya taasisi na kufikia malengo ya kimkakati katika kuboresha huduma bora katika viwanja vya ndege na usafiri kwa anga kwa jumla.

Mafunzo hayo ni muendelezo wa kuwajengea uwezo Bodi na Menejimenti ya Mamlaka katika kutekeleza wajibu wake wa kusimamia mabadiliko ndani ya taasisi na kufikia malengo ya kimkakati katika kuboresha huduma bora katika viwanja vya ndege na usafiri kwa anga kwa jumla.

"Mafunzo haya yametupa mtazamo mpya kuhusu namna bora ya kuongoza taasisi kubwa kama TAA kwa uwazi, nidhamu na ubunifu. Tunapaswa sasa kuyageuza mafunzo haya kuwa vitendo vinavyoleta matokeo halisi katika usimamizi wa viwanja vyetu vya ndege na huduma tunazotoa kwa Watanzania," amesema Bw. Fimbo.

Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania inaendelea kuwekeza katika mafunzo ya viongozi na watumishi wake ili kuhakikisha huduma bora, salama na endelevu zinatolewa katika viwanja vyote vya ndege nchini.

Akifunga mafunzo hayo, Mwenyekiti wa Bodi ya TAA, Bw. Juma Hassan Fimbo, amewapongeza wajumbe wote kwa ushiriki wao wa dhati na kusisitiza umuhimu wa kuyatumia mafunzo hayo katika kuboresha utendaji wa kila siku.nia," alisema Bw. Fimbo

Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania inaendelea kuwekeza katika mafunzo ya viongozi na watumishi wake ili kuhakikisha huduma bora, salama na endelevu zinatolewa katika viwanja vyote vya ndege nchini. Bunju jijini Dar es Salaam.

Akifunga mafunzo hayo, Mwenyekiti wa Bodi ya TAA, Bw. Juma Hassan Fimbo, aliwapongeza wajumbe wote kwa ushiriki wao wa dhati na kusisitiza umuhimu wa kuyatumia mafunzo hayo katika kuboresha utendaji wa kila siku.





# TAA YALIPA FIDIA WANANCHI WANAOPISHA UJENZI WA KIWANJA CHA NDEGE CHA MUSOMA

Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania (TAA) imeanza zoezi la ulipaji fidia kwa wananchi wa Mtaa wa Kamnyonge Bondeni, mkoani Mara, ili kupisha ujenzi wa jengo la abiria katika Kiwanja cha Ndege cha Musoma

Bi. Comino alieleza kuwa hadi sasa ujenzi wake umefikia asilimia 58, na kukamilika kwake kunatarajiwa kufungua fursa nyingi za kiuchumi, hususani katika sekta ya utalii

Meneja wa Kanda ya Ziwa wa TAA, Bi. Rose Comino, amesema Serikali imetenga zaidi ya shilingi bilioni 5 kwa ajili ya ulipaji wa fidia kwa wananchi wanao pisha mradi huo.

Bi. Comino ameongeza kuwa hadi sasa mradi umefikia asilimia 58, na kukamilika kwake kunatarajiwa kufungua fursa nyingi za kiuchumi, hususani katika sekta ya utalii.

Kwa upande wake, Mkuu wa Wilaya ya Musoma, Mheshimiwa Juma Chikoka, amewataka wananchi kuhakikisha wanazingatia makubaliano yaliyofikiwa baada ya kupokea malipo yao, ili kuruhusu utekelezaji wa mradi kuendelea kwa kasi na ufanisi.

Aidha, Mhe, Chikoka amewahimiza wananchi wa eneo hilo kujiandaa kuchangamkia fursa zitakazotokana na kukamilika kwa kiwanja hicho, ikiwemo ukuaji wa sekta ya biashara, ajira, na ongezeko la wageni watakaokuwa wakifika mkoani humo

"Kukamilika kwa Kiwanja cha Ndege cha Musoma kutachochea maendeleo ya kiuchumi katika Mkoa wa Mara, kwani kutarahisisha usafiri wa anga, kuongeza mzunguko wa biashara, na kuimarisha sekta ya utalii," alisema Chikoka.








# MRADI WA UKARABATI NA UPANUZI WA KIWANJA CHA NDEGE CHA IRINGA

Chini ya uongozi wa Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Serikali ya Awamu ya Sita inaendelea kutekeleza kwa mafanikio makubwa miradi ya kimkakati ya miundombinu ya usafiri wa anga, ikiwa ni pamoja na Mradi wa Ukarabati na Upanuzi wa Kiwanja cha Ndege cha Iringa kwa gharama ya zaidi ya Bilioni 63.

Kupitia mradi huu, barabara ya kuruka na kutua ndege imeboreshwa kutoka urefu wa mita 1,679 na upana wa mita 30 hadi kufikia mita 2,100 yenye upana wa mita 30, kwa kiwango cha lami. Uboreshaji huu umeongeza usalama, uimara na uwezo wa kiwanja kupokea ndege kubwa zaidi kwa wakati wote.

Aidha, mradi umehusisha ujenzi wa njia unganishi yenye urefu wa mita 155, pamoja na ujenzi wa maegesho ya ndege yenye upana wa mita 126 na urefu wa mita 180, hatua inayorahisisha shughuli za uendeshaji wa ndege.

Vilevile ujenzi wa uzio wa usalama wenye urefu wa kilomita 10, ujenzi wa kituo cha umeme, na uwekaji wa jenereta lenye uwezo wa kufua umeme wa 450 KVA, ili kuhakikisha upatikanaji wa nishati ya uhakika kwa shughuli zote za kiwanja.

Pamoja na hayo, mradi umehusisha ujenzi wa kituo cha zimamoto, ununuzi wa gari la kisasa la zimamoto, usimikaji wa taa za kuongozea ndege, hatua ambayo inarahisisha na kuwezesha ndege kutua na kuruka kwa usalama nyakati zote, mchana na usiku.mchana na usiku.

Hadi sasa, utekelezaji wa mradi huu umefikia asilimia 98 na asilimia 10.5 za ujenzi wa Jengo jipya la kudumu la abiria.



# MATUKIO KATIKA PICHA




Naibu Waziri wa Uchukuzi, Mhe. David Mwakiposa Kihenzile alipotembelea banda la Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania (TAA) katika maonesho ya Wiki ya Utumishi wa Umma. Chinangali Park, Dodoma.



Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Viwanja vya ndege Tanzania Bw. Abdul Mombokaleo akiwa na Menejimenti ya TAA na baadhi ya watumishi katika hafla ya kuwaaga watumishi waliostaafu, Jijini Dar es Salaam.




Watumishi wanawake kutoka Mamlaka ya Viwanja vya ndege Tanzania(TAA) na kiwanja cha ndege cha Kimataifa cha Julius Nyerere wametoa msaada katika gereza la wanawake segerea ikiwa ni sehemu ya utamaduni wa kurudisha kwa jamii



Mwenyekiti wa Bodi ya Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania (TAA) Bw. Juma H. Fimbo, pamoja na Mkurugenzi Mkuu wa TAA Bw. Abdul Mombokaleo, watia saini mkataba wa utekelezaji na utendaji kazi kwa mwaka wa fedha 2025/2026, Makao Makuu ya Mamlaka ya Viwanja vya ndege Tanzania.




Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania yapokea tuzo ya ACI Afrika 2025 kwa Ubora wa Huduma katika Viwanja vya Ndege, hii inathibitisha dhamira ya taasisi katika utoaji huduma zenye viwango vya kimataifa.




Kiwanja cha ndege cha Kimataifa cha Julius Nyerere chapokea tuzo ya World Travel Award kwa kuwa kiwanja bora cha Ndege barani Afrika kwa mwaka 2025 katika utoaji huduma bora.


Tanzania Airports Authority
FURAHIA SAFARI YAKO
GARI LAKO LIKIWA MIKONONI MWETU
ELFU 15000/= Kwa saa 24
Usalama wa gari lako
Mikononi mwetu pindi uwapo safarini
Huna haja ya kukodi USAFIRI
Njoo na gari lako tutakuhifadhia kwa gharama nafuu
15000 /= Kwa Saa 24
+255 22 2842402/3
info@airports.go.tz
www.taa.go.tz
@tanzaniairports

# WATU WETU



BW. SHABAN YAHYA DOGOLI

Bw. Shaban Yahya Dogoli aliyestaafu Utumishi wa Umma ndani ya Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania (TAA) kwa mujibu wa sheria na taratibu za utumishi mnamo 26 Januari 2026. Safari yake ya utumishi haikuwa rahisi; ilijaa changamoto nyingi, misukosuko ya kukatisha tamaa, na mazingira magumu ya kazi. Hata hivyo, uvumilivu wake, uadilifu, na kujituma vilimfanya aendelee kusonga mbele hadi ilipofikia kustaafu kwake.

**Safari yake ya Kikazi;**
Bw. Dogoli, mkazi wa Buguruni Ilala Dar es Salaam, alianza safari yake ya utumishi mwaka 1984, akiajiriwa kama Mhudumu wa kawaida wakati huo, TAA ikijulikana kama Directorate of Aerodromes chini ya Wizara ya Ujenzi,

Amesimulia kuwa kipindi hicho kazi nyingi zilifanywa kwa njia ya analojia bila msaada wa teknolojia yoyote, huku malipo ya mshahara yakiwa madogo kwa takribani shilingi 600 bila posho yoyote ya kujikimu. Ugumu huu uliwakatisha tamaa watumishi wengi alioanza nao utumishi na wengi waliamua kuacha kazi. Lakini yeye alibaki, akavumilia, akafanya kazi kwa uaminifu, na akajenga msingi wa utendaji uliomfikisha mpaka sasa.

Katika kipindi hicho kigumu, ushauri kutoka kwa mke wake ulimpa nguvu ya kuendelea: “Kila nilipoonesha kukata tamaa, mke wangu alikuwa akinitia moyo.” Ameeleza Bw. Dogoli. Ushirikiano katika familia ulikuwa nguzo muhimu iliyomsukuma kusonga mbele.

**Tuzo na Mafanikio;**
Jitihada za muda mrefu za Bw. Dogoli hazikupotea na mwaka 1993, katika maadhimisho ya Mei Mosi, alitunukiwa Cheti cha Mfanyakazi Bora wa Mwaka wa iliyokuwa Directorate of Aerodromes, sambamba na zawadi ya shilingi 70,000.Tukio hilo lilimpa hamasa mpya na kumfanya azidi kupenda kazi yake ya uhudumu katika ofisi.

**Mabadiliko ya Taasisi;**
Baada ya miaka kadhaa, jina la taasisi lilibadilishwa kutoka Directorate of Aerodromes na kuwa Dar es Salaam International Airport (DIA). Mabadiliko hayo, sambamba na ongezeko la maslahi, yaliimarisha zaidi ari yake ya kazi.Uaminifu na ubora wa utendaji wa Bw. Dogoli ulimfanya kuaminiwa na kupewa jukumu la kupanga majukumu ya watumishi wenzake, pamoja na kuandaa makabrasha muhimu ya taarifa zilizokuwa zikitumika katika Baraza la wafanyakazi.

Bw. Dogoli amestaafu na cheo cha Mhudumu Mwandamizi wa Ofisi, cheo alichokifikia kutokana na juhudi na historia ndefu ya utendaji wa mfano.

**Changamoto za Kazi;**
Mbali na changamoto za mishahara midogo na mazingira duni ya kazi katika miaka hiyo, anasema kukosekana kwa vifaa vya kisasa kulileta ugumu katika kutekeleza majukumu kwa wakati. Hata hivyo, alibaki mtiifu, mwenye nidhamu, na mwenye uwezo wa kubadilika kulingana na mageuzi ya taasisi.

**Mambo Asiyoyasahau;**
Kwenye safari yake yote ya utumishi, tukio la kukumbukwa zaidi kwake ni tuzo aliyopewa mwaka 1993 na Cheti cha Mfanyakazi Bora jambo ambalo anasema limebaki kuwa alama muhimu ya safari yake ya kikazi

**Ushauri wake;**
Bw. Dogoli anasisitiza umuhimu wa serikali na taasisi zake kuandaa mazingira rafiki kwa watumishi wanaokaribia kustaafu, ili kuhakikisha wanapata mafao yao kwa wakati na kuepusha usumbufu usio wa lazima.



Aidha, anatoa wito kwa watumishi wote kuwa watunzaji wa siri za ofisi na kuepuka utoaji holela wa taarifa, jambo linaloharibu taswira na uaminifu wa mtumishi wa umma. Anahimiza pia uvumilivu, kuipenda kazi, na kujenga umoja miongoni mwa watumishi.

**Shukrani;**
Kwa unyenyekevu mkubwa, Bw. Dogoli anawashukuru viongozi wa TAA kwa jitihada zao katika kuboresha maslahi ya watumishi na kwa mageuzi makubwa ya kiteknolojia yaayoendelea kuleta tija katika utendaji na utoaji huduma.Anasema safari yake ya utumishi imekuwa somo, baraka, na fahari na sasa anaingia kwenye ukurasa mpya wa maisha ya kupumzika baada ya kulitumikia Taifa kwa uaminifu kwa karibu miaka 42.